MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na. 31. Msimu wa Kilimo 2021/22* *Tathmini ya Julai 21-31, 2022 na Matazamio kwa Kipindi cha Agosti 1-10, 2022*

**MUHTASARI**

- Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa, wafugaji wanashauriwa kutumia maji na malisho kwa uangalifu.
- Mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa hususan katika mikoa ya Pwani zinaweza kuathiri mikorosho iliyo katika hatua ya kutoa maua.
- Wakulima hususan wa maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka wanashauriwa kuanza shughuli za kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu mvua za ***Vuli***.


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 21-31, 2022

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii iliendelea kuimarisha ukanda wa mgandamizo mkubwa wa hewa katika baadhi ya maeneo na hivyo kuleta mchango katika kusukuma hewa yenye ubaridi kuelekea katika baadhi ya maeneo nchini ikiwa ni pamoja na kuimarisha mwendokasi wa upepo.

Joto la bahari katika eneo kubwa la bahari ya Hindi lilikuwa la wastani hadi chini ya wastani, hali ambayo ilikuwa na mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya mwambao wa pwani ya nchi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 21-31, 2022

Katika kipindi hiki, maeneo machache ya mikoa ya Kagera, Mara na Mwanza, mwambao wa pwani vikiwemo visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia pamoja na maeneo kuzunguka Ziwa Manyara, Eyasi, Natron pamoja na Ziwa Rukwa yalipata vipindi vya mvua za nje ya msimu. Maeneo mengine yaliyosalia yalikua makavu kwa ujumla kama inavyoonekana kwenye kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Julai 21-31, 2022

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 21-31, 2022

Katika dekadi hii maeneo machache nchini yalipata vipindi vya mvua wakati maeneo mengi ya nchi yalikuwa makavu kwa ujumla.

Kwa maeneo yanayopata mvua za msimu, mazao ya mahindi, mpunga na alizeti yalikuwa katika hatua ya kukomaa na kukauka ambapo wakulima waliendelea na shughuli za uvunaji wa mazao hayo.

Kwa upande wa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan mikoa ya mwambao wa Pwani, yalipata mvua ambayo ilisaidia katika upandaji wa mihogo. Maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyamapori yamepungua kidogo kutokana na hali ya ukavu inayoendelea nchini.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 21-31, 2022

Kwa ujumla hali ya maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito na mabonde ilikuwa ya kawaida katika mabonde mengi nchini.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 1-10, 2022

Katika dekadi hii, tunatarajia migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini ikiendelea kupungua nguvu.

Hali hii itaendelea kuimarisha ukanda wa mgandamizo mkubwa wa hewa katika baadhi ya maeneo nchini na hivyo kuchangia katika kusukuma hewa yenye ubaridi kuelekea katika baadhi ya maeneo.

Joto la bahari katika eneo kubwa la bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini ya wastani, wakati eneo la kati la bahari ya Pasifiki joto la bahari linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani hali ambayo haitakuwa na mchango katika kuchochea visababishi vya mvua nchini.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 1-10, 2022

Maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu, na Mara) yanatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya mvua na ngurumo za radi husussan katika nusu ya kwanza ya dekadi.

Maeneo ya magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) inatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya mvua katika maeneo machache.

Maeneo ya pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kuwa makavu yakiambatana na hali ya ubaridi pamoja na vipindi vifupi vya mvua nyepesi.

Maeneo ya kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla yakiambatana na hali ya ubaridi.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KIPINDI CHA AGOSTI 1-10, 2022

Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia shughuli za uvunaji, ukaushaji na uhifadhi wa mazao.

Hata hivyo, hali hii ya ukavu inaweza kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya wanyama.

Mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa hususan katika mikoa ya mwambao wa pwani zinaweza kuathiri mikorosho iliyo katika hatua ya kutoa maua, na pia zitasaidia ukuaji wa mihogo iliyopandwa.

Baadhi ya maeneo nchini yanatarajiwa kuwa na hali ya ubaridi. Hali hii inaweza kuwa na athari kwa mazao na wanyama pia kuathiri upatikanaji wa samaki.

Wavuvi wanashauriwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.

Wakulima hususan kwa maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, wanashauriwa kuanza shughuli za kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu mvua za vuli.

Kwa ujumla inashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 1-10, 2022

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa katika hali ya kawaida katika mabonde nchini, isipokuwa katika bonde la Ziwa Victoria na maeneo machache ya bonde la Wami-Ruvu ambayo yanatarajiwa kuwa na ongezeko kidogo la maji.

Watumiaji wa maji wanashauriwa kuyatumia kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*
**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**
**Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro.**
*S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz*, -Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania